

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/58

Fax: +25522203213

Tovuti: www.dsm.go.tz

Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA

3 Barabara ya Rashidi

Kawawa,

S.L.P 5429,

12880 -DAR ES SALAAM.

Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**RC MAKONDA AWATEMBELEA WAHANGA WA MAFURUKO DAR, AWATAKA
WANANCHI KUCHUKUWA TAHDHARI**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mheshimiwa PAUL MAKONDA leo amefanya Ziara ya kukagua miundombinu iliyothiriwa na Mafuriko yaliyotokana na Mvua zinazoendelea kunyesha na kusema Serikali itakarabati mara moja miundombinu yote iliyothiriwa na Mvua.

Katika ziara hiyo RC MAKONDA ameambatana na Kamati ya Maafa ya Mkoa ambapo wametembelea maeneo mbalimbali yaliyothiriwa na Mvua ikiwemo Jangwani, Daraja la Malecela, Daraja la Korongo, Daraja la Tandale kwa Mtogore, Africana na Boko Basihaya na kutoa pole kwa Wahanga.

Akizungumza na Wananchi hao RC MAKONDA amewataka Wananchi waliojenga kwenye maeneo hararishi kuchukuwa tahadhari mapema kwakuwa Wataalamu wa hali ya Hewa wametangaza kuwa Mvua kubwa zitaendelea kunyesha.

Amesema kuwa Ujenzi wa Miundombinu iliyoharibiwa ikiwemo ya Maji, Umeme, Mitaro, Barabara na Madaraja inaendelea ambapo kwenye Daraja la Malecela ameagiza kujengwa Daraja la Muda mfupi chini ya Vijana kutoka Jeshi la Wananchi.

RC MAKONDA amesema kuwa zaidi ya Shilingi Billion Moja zimetolewa na Bank ya Dunia kwa ajili ya Maboresho ya eneo la Jangwani ambapo amesema Serikali ya Mkoa ina vifaa vya kutosha kwa ajili ya kuokoa Wananchi.

Aidha RC MAKONDA amesema kuwa mionganini mwa sababu zilizopelekeea Maji ya mvua kukosa mwelekeo ni Ujenzi holela, Uchimbaji wa Mchanga na watu kutupa Uchafu kwenye Mito.

Mionganini mwa Wilaya alizotembelea RC MAKONDA ni pamoja na Ilala, Ubungo na Kinondoni ambapo kuna nyumba zaidi ya 200 zipo kwenye mazingira hatarishi.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

28/10/2017